

Swahili

Usalama wa Fukwe



No Flags

No Swim

Hakuna Bendera

Usiogeelee

**Huduma ya Walinzi
wa Kuogelea**

Kukuweka salama



- Wakati wote ogelea kati ya bendera nyekundu na ya manjano (bendera hizi zinaonyesha eneo lililoteuliwa la kuogelea).
- Ogelea tu kwenye fukwe zinazolindwa doria na walinzi na waokozi wa kuogelea.
- Iwapo ukipata shida, tulia na inua mkono wako.
- Wakati wote uwasimamie watoto.
- Usiogelee peke yako.
- Fuata ushauri wa walinzi na waokozi wa kuogelea.
- Wakati wote vaa kofia, miwani ya jua, shati na mafuta ya kuzuia jua. Kunywa maji mengi.
- Kamwe usinywe pombe na kuogelea.



Fukwe Zinazolindwa na Walinzi wa Kuogelea

Fukwe zote 17 zinalindwa doria kuanzia mwanzo wa Likizo za Shule za NSW katika mwezi wa tisa (Septemba) hadi mwisho wa likizo za Shule mwezi wa nne (Aprili). Ufukwe wa North Wollongong upo wazi mwaka mzima.

Angalia tovuti ya Halmashauri ili kupata habari zaidi juu ya mahali pa ufukwe, masheria, ubora wa maji na jinsi ya kupata matumizi ya kiti cha gurudumu cha fukwe.



kuogelea katika eneo linalolindwa doria na walinzi wa kuogelea



usiogelee wakati bendera nyekundu zipo



kupanda ubao wa kuteleza kwenye mawimbi hakuruhusiwi



onyo ya wenye mwiba



mbwa ni marufuku



usitupe takataka

Walinzi na Waokozi wa kuogelea

Walinzi wa kuogelea wanatumwa na Halmashauri ya Manispaa ya Wollongong kwenye fukwe na mabwawa. Wanavaa shati nyeupe na captura bluu bahari. Walinzi wetu wa kuogelea wanafanya doria kwa kawaidia kuanzia Jumatatu (Monday) hadi Jumamosi (Saturday).

Waokozi wa kuogelea ni watu wanaojitua muda wao kufanya doria kwenye fukwe Jumapili (Sunday) na Likizo za Umma. Wanavaa sare nyekundu na manjano.



Mbao wa kuteleza kwenye mawimbi zisitumiwe kati ya bendera nyekundu na ya manjano.



Waokozi wa kuogelea wa hiari.

Mikondo ya Mpasuko

Fukwe nyingi zina mipasuko. Mipasuko husukuma maji kurudi hadi baharini na kubeba vitu vinavyoelea, ikiwa ni pamoja na watu, navyo. Baadhi ya ishara za mpasuko ni pamoja na:

- Maji yenye rangi nzito yasiyo na mawimbi yanayopasuka au mawimbi machache.
- Uso wenye wimbi kuzungukwa na maji laini.
- Sio mipasuko yote huonyesha ishara zote hizi. Iwapo una mashaka, kaa nje ya maji.
- Iwapo ukishikwa na mpasuko, usijaribu kuogelea dhidi yake. Ukianza kuchoka, jaribu kuelea.

Mpango Wetu wa Elimu

Iwapo ungependa Wollongong Lifeguard Service kuja shuleni kwako au kama utataka maelezo zaidi uwasiliane nasi.

Habari

Kupata habari zaidi tembelea tovuti ya 'Beaches' ya Halmashauri au pigia simu kwa Huduma ya Wateja kwenye (02) 4227 7111.

Iwapo ukihitaji mkalimani piga simu kwa Huduma ya Mkalimani wa Simu kwenye 131 450 na uombe kuwasiliana na Wollongong City Council Customer Service.

Tembelea Mkondo wa Wollongong City Council YouTube ili kuangalia video za usalama wa kuteleza kwa ubao kwenye mawimbi.

www.wollongong.nsw.gov.au/lifeguards